

UNAWEZA KUSIMAMA TENA



Mwalimu: John James



Muhtasari

LIVE

YALIYOMO / OUTLINE

Vizuizi vya Kusimama Tena

Kanuni ya Kupanda Juu




By: Mwalimu: John James



BWC

2



Mika 7:8

Usifurahi juu yangu, Ee **Adui** yangu;
NIANGUKAPO, NITASIMAMA tena; nikaapo
gizani, Bwana atakuwa nuru kwangu.

Utangulizi wa Kitabu cha Mika

— 700-900 BC

“**Mika**” katika lugha ya Kiebrania ni kifupisho cha jina
“**Mikaya**”, maana yake “**ni nani aliye kama BWANA?**”



“**Mika**” alifanya kazi na Manabii:

Hosea, Amosi na Isaya

“**Mika**” alifanya kazi chini:

Yotham, Ahazi na Hezekia

— Mwefraimu

— Mwana wa Imla (Mikaya) Aliyechukiwa na Mfalme **Ahabu**

— Mmorashi Gath; na ndiye Starring Hapa

Israel, Kaskazini (10) Samalia

Yuda, Kusini (2) Yerusalemu

Alitoka Familia ya Wakulima na Wafugaji ambao walinyanyaswa kwa sababu ya dhuluma kubwa.

40 km from Yerusalem



Historia:

“**ISAYA** alitabiri Kuzaliwa kwa Yesu na Bikira Malia Lakini
MIKA alitabiri alikozaliwa YESU Yaani Bethlehem **(5:2)**, Nabii wa kwanza kutabiri Yerusalemu kubomolewa na na anguko na kwenda utumwani BABELI

Serikali ilizidi kwa dhuluma, Manabii wa uongo waliungana kwa wizi na rushwa na kukandamiza wengi waliokuwa wakulima na wafugaji kwani ardhi ilikuwa inamilikiwa na watu wachache. Dhuluma ilizidi na watu wachache wa Mungu kama Manabii wakapigwa vita sana na Viongozi wa Dini ambao walikuwa wamemezwa na Siasa kwa Kumchukia na kuwa kinyume na yeyote aliyetabiri kinyume na Serikali. ”



Ufisadi wa kiadili na ibada ya sanamu ni mambo yaliyokuwa yamekolea katika Israeli, na jambo hilo likaletea taifa hilo uharibifu kutoka **Ashuru**



Fikiria mwanamume mwenye ujasiri, anatabiri mbele ya mafisadi na viongozi wa nchi Akisema

Mika 3:3 Naam, **mnakula nyama** ya **watu** wangu, na kuwachuna ngozi **zao**, na kuivunja mifupa yao; naam, kuwakata vipande vipande kama kwa kutiwa chunguni, na kama **nyama** sufuriani.





Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda **haki**, na **kupenda rehema**, na kwenda kwa **unyenyekevu** na Mungu wako! **MIKA 6:8**

7

www.micahcommunitychurch.org

KANISA LA JAMII LA MIKA **Haki Rehema Unyenyekevu**



[Micah Community Church | Horace, North Dakota](http://www.micahcommunitychurch.org)




Mika 7:8

Usifurahi juu yangu, **EE ADUI** yangu;
NIANGUKAPO,NITASIMAMA tena; nikaapo
gizani, Bwana atakuwa nuru kwangu.

Isaya 60:1

Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako
imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia.






**HATMA YA NURU
YA BWANA
ISAYA 60:1**




Yeremia 29:11 Maana **NAYAJUA MAWAZO** ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni **MAWAZO** ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.



**HATMA YA NURU
YA BWANA
ISAYA 60:1**




Yeremia 29:11 Maana **NAYAJUA**
MAWAZO ninayowawazia ninyi,
asema Bwana, ni **MAWAZO** ya amani
wala si ya mabaya, kuwapa ninyi
tumaini siku zenu za mwisho.



NURU YA BWANA


ISAYA 60:1



Yeremia 29:11 Maana **NAYAJUA**
MAWAZO ninayowawazia ninyi,
asema Bwana, ni **MAWAZO** ya amani
wala si ya mabaya, kuwapa ninyi
tumaini siku zenu za mwisho.


12





NURU YA BWANA


ISAYA 60:1



Yeremia 29:11 Maana **NAYAJUA**
MAWAZO ninayowawazia ninyi,
asema Bwana, ni **MAWAZO** ya amani
wala si ya mabaya, kuwapa ninyi
tumaini siku zenu za mwisho.


13





NURU YA BWANA


ISAYA 60:1




Yeremia 29:11 Maana **NAYAJUA**
MAWAZO ninayowawazia ninyi,
asema Bwana, ni **MAWAZO** ya amani
wala si ya mabaya, kuwapa ninyi
tumaini siku zenu za mwisho.

14






NURU YA BWANA ISAYA 60:1



Yeremia 29:11 Maana **NAYAJUA**
MAWAZO ninayowawazia ninyi,
asema Bwana, ni **MAWAZO** ya amani
wala si ya mabaya, kuwapa ninyi
tumaini siku zenu za mwisho.

15





NURU YA BWANA

ISAYA 60:1

Yeremia 29:11 Maana **NAYAJUA**
MAWAZO ninayowawazia ninyi,
asema Bwana, ni **MAWAZO** ya amani
wala si ya mabaya, kuwapa ninyi
tumaini siku zenu za mwisho.

16





HARAKATI ZA MAISHA YA MTU





Mhubiri 3:4

Wakati wa kulia, na wakati wa kucheka;
Wakati wa kuomboleza, na wakati wa
kucheza.....



LIVE

**Vizuizi vya
Kusimama Tena**

Utangulizi





Maisha ya mwanadamu yamejaa milima na mabonde na kila mtu lazima apitie kwa namna moja ama nyingine.....

20

Raha, Baraka, Mafanikio

Uzima, Ushindi, Amani

Kuinuliwa, Kibali.....

Taabu, Kilio, Machozi

Kukata Tamaa, Hasara

Kupoteza, Majanga.....

Kuhukumiwa, Kusemwa

1: Usijitambue wewe ni nani?

- 1 Kiumbe wa Kiroho Aishiye kwenye Nyumba litwayo Mwili, Mungu ni roho pia.....
- 2 Ni sura ya Mungu, Hivyo Mungu ni Mtakatifu na Mimi ntakuwa Hivyo.
- 3 Hekalu la Mungu kwa kuwa roho wa Mungu anakaa ndani yako.
- 4 Ni balozi wa Mungu na Ufalme wa Mungu, Hivyo nimeitwa kuwa kinyume na Ufalme wa Giza

KUMBUKA

Hatima yako imefichwa ulimwengu usionekana na ndio huitwa Ulimwengu wa roho! (Huku ndiko Huitwa Ulimwengu wa roho)

- MAWAZO YAKO.....Mindset
- MTAZAMO WAKO.....Attitude
- FIKRA ZAKO.....Thinking
- UFAHAMU WAKO.....Knowledge
- UTASHI WAKO.....



Ebrania 11:3

Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu **vilivyo dhahiri**.

Mith 4:23

Linda moyo wako kuliko yote uya**linda**yo; Maana ndiko zitokako chemchemi za uzima.

MAWAZO + MTAZAMO + FIKRA + UFAHAMU

= MOYO (rohoni). Utashi, Nia, Nafsi

KUMBUKA

Ulimwengu Usionekana (roho) ndio Uliumba Ulimwengu unaonekana

→ Utajiri ni Mtazamo, **na Umasikini ni Mtazamo**

→ Utajiri ni Maarifa, **Umasikini ni Kukosa
Maarifa**

→ Utajiri ni Wingi wa Mawazo chanya,
Umasikini ni wingi wa mawazo hasi

→ Kushinda, kuinuka, Kusimama ni Mtazamo,
Kushindwa, Kubaki chini, Ni Mtazamo

1 Wakorintho 3:16

Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa **hekalu** la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?

25



2: Usimtambue Adui yako



**Chochote kinachoweza
Kukuzuia wewe
Usiwe vile ungependa kuwa**

1 PETRO 5:8 Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu **Ammeze**

ADUI YAKO ANAKU SABABISHIA NINI?



Usifanye kazi zako na Ukafanikiwa



Usimtumikie Mungu kwa Furaha



Usimwabudu Mungu wako



Usitimize Malengo yako



Mungu asijifunue kwako



Usimfurahie Mungu



Usifurahie Baraka /Mafanikio yako





Yohana 10:10

Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.

Warumi 7:19-20

Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo **nilitendalo**. Basi kama lile nisilolipenda ndilo **nilitendalo**, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu.



MAKUNDI YA MAADUI ZAKO

- Aliye ndani yako.... Magonjwa
- Wewe mwenyewe...Mtizamo
- Wanadamu.....Watu
- Shetani.....Pepo

1 Petr 5:8

Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu **ammeze**.

Shetani anataka usimjue ili ushindwe Vita

- Anataka Ugombane na Mungu (Hajakusaidia), kwa kususia kufanya mapenzi yake.
- Anataka ugombane na wanadamu na sio shetani (uwaweke watu moyoni).
- Anataka ufanye vita kwa jinsi ya Mwili, ili Ujihakikishie kushindwa.

2 Wak 10:3

30

Maana ingawa tunaenenda katika mwili, **hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili;**



MFANO WA MAADUI NDANI YAKO

Uzembe, Hofu, Uvivu

Kutofanya kazi, Bidii

Kujihurumia

Kukata Tamaa

Woga, Ujinga

Magomvi

Dhambi



Ewe mvivu, mwendee **chungu**, Zitafakari njia zake ukapate hekima.

Mith 6:6



32





Efeso 5:16

Waefeso 5:16 mkiukomboa wakati
kwa maana zamani hizi ni za uovu.

Kolosai 4:5

Wakolosai 4:5 Enendeni kwa
hekima mbele yao walio nje,
mkiukomboa wakati.





SIFA ZA MTU ANAYEMTAMBUA ADUI YAKE

- Hawezi kamwe kumlaumu Mungu wala wanadamu wala kumnung'unikia bali mtu wa Shukrani.**
- Anafanya vita kwa jinsi ya rohoni na si mwilini yaani kugombana na watu maana anapingana na nguvu iliyo nyuma ya hao watu.**



Math 16:23

Akageuka, akamwambia Petro, Nenda **nyuma yangu, Shetani;** u kikwazo kwangu; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu. **(Alikuwa katika roho akiongea na roho mbaya iliyokuwa ndani ya petro ikifanya vita na kusudi la Mungu kutukomboa)**

Ufun 12:11

Nao wakamshinda kwa **DAMU** ya Mwana-Kondoo, na kwa **NENO** la **USHUHUDA WAO;** ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.



2 Wak 10:3-5

3 Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya **mwili**;

4 (maana silaha za vita vyetu **si za mwili**, bali **(ni za roho)** zinauwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;)

5 tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila **FIKIRA** / **NIA** ipate kumtii Kristo.

3: Ujione uko Pekee yako

Tatizo lako ni jipya na halijawahi kutokea duniani ama katika jamii ama kanisani, Hivyo hata cha kufanya Hakuna, Wewe ni wa kufa na kufeli tuu, Masikini tuu na kamwe usisumbuke/Usisumbue watu.



Mhub 1:9

38 Yaliyokuwako ndiyo yatakayokuwako; na yaliyotendeka ndiyo yatakayotendeka; wala jambo jipya hakuna chini ya jua

● Isaya 49:16

Tazama, **nimekuchora** katika vitanga vya mikono yangu; kuta zako ziko mbele zangu daima.

Kuto 23:20

Tazama, mimi namtuma **malaika** aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengezea.

Alikuwa na Danieli kwenye tundu la simba

Mungu atakuwa nawe katika hiyo hali yako

Daima Mungu hamwachi mtu kabisa

4: Kujihukumu na Kukata Tamaa

Kwa hali yako hiyo uliyonayo
usitegemee chochote
tena.....

Kol 2:14

Akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea **msalabani**



KUMBUKA

Unapojihukumu, Unatangaza Kujichoma Msumari Mrefu na Mkubwa kuliko Ule uliomsulubisha Yesu Msalabani



41

UJIHUKUMU MWENYEWE

SHETANI AKUHUKUMU

WATU WAKUHUKUMU

MUNGU AKUHUKUMU

DUNIA IKUHUKUMU





USIJHUKUMU MWENYEWE



42

USIKATE TAMAA

! IMPORTANT

TABIA ZA MTU ANAYEJIHUKUMU

KUMBUKA

Hana Furaha na Amani

Anakata Tamaa tuu

Hawezi Msifu Mungu

Ana roho ya uchungu

Hawezi Mfurahi Mungu na watu

Anajiwekea Muhuri wa Kushindwa

5: Kuwa Mvivu na Kujihurumia

‘Umechelewa, Una kiasi kidogo sana, Mtaji wako ni Mdogo sana, Una Elimu ndogo, Ahirisha tuu kwenda, Mvua ni Kali lala tuu.



44

Acha tuu, Mtaji Mdogo

Ahirisha tuu, Usianze !!

Usiende kabisa kanisani

Usijaribu Tena




Umeamka saa 3
unasema huendi
kanisani wakati
unaweza ukaenda na
ukafika neno bado
halijaanza?

roho za kubaki hapo
hapo ulipo pia ni za
kuweka vipolo.

6: Kutoridhika na Manung'uniko

Wapendwa wa siku hizi Bwana hawana Upendo, ukiwaomba Wakusaidie hawakusaidii kwa moyo kwa 100 %. **Akikopa halipi kwa maana huamini amesaidiwa,** na ole umdai atakutangaza una roho mbaya.



7. Kuishi bila Mipango/Malengo

- ✓ Jifunze kuwa ni Mtu wa Maono na Dira
- ✓ Weka Malengo yako kwa Muda fulani
- ✓ Tekeleza huku Ukiongozwa na Mungu
- ✓ Fanya Tathmini, Mshukuru na Jipange Upya
- ✓ Usiwe mtu unayebadiriika badirika
Utamchanganya Mungu na Jamii yako





Hab 2:1-3

1 Mimi nitasimama katika zamu yangu, nitajiweka juu ya mnara, nitaangalia ili nione atakaloniambia, na jinsi nitakavyojibu katika habari ya kulalamika kwangu.

2 Bwana akanijibu, akasema, landike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji.

3 Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia.